

TOLEO RAHISI LA MKAKATI WA TAIFA WA KILIMO IKOLOJIA HAI 2023-2030

1. Utangulizi

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania. Kinatoa chakula, ajira, kipato na malighafi kwa viwanda. Hata hivyo, kilimo kinakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwemo:

- i. Mabadiliko ya tabianchi;
- ii. Ukame na mvua zisizotabirika;
- iii. Kupungua kwa rutuba ya udongo;
- iv. Kuongezeka kwa wadudu, magonjwa na magugu;
- v. Kupotea kwa mbegu na mifugo ya asili;
- vi. Gharama kubwa za pembejeo;
- vii. Masoko yasiyo ya uhakika;
- viii. Uelewa mdogo kuhusu kilimo hai na kilimo ikolojia hai.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kilimo Ikolojia Hai (NEOAS) kwa kipindi cha 2023–2030.

2. Mkakati wa Kilimo Ikolojia hai unahusu nini?

Mkakati wa Taifa wa Kilimo Ikolojia Hai (NEOAS) ni mpango wa miaka nane wa Tanzania wa kuhimiza uzalishaji wa chakula kwa kuzingatia afya ya Udongo, Maji, Mimea, Wanyama, Binadamu, na Mazingira kwa ujumla. Mkakati huu unalenga kuzalisha chakula salama kwa kutumia rasilimali za asili kwa uangalifu na kupunguza utegemezi wa kemikali za viwandani. Mkakati huu unahimiza kilimo kinachoendana na asili badala ya kwenda kinyume nayo.

NEOAS inaunganisha maarifa ya jadi ya kilimo na sayansi ya kisasa ili kuwasaidia wakulima: Kuzalisha chakula salama na chenye lishe; Kuboresha afya ya udongo na kulinda vyanzo vya maji; Kupunguza utegemezi wa pembejeo za gharama kubwa kutoka nje; Kuhifadhi bayoanuwai na mbegu za asili; Kukabiliana na ukame, mafuriko na mabadiliko ya hali ya hewa; Kuongeza mapato ya kaya na ajira; na Kupata masoko bora ya ndani, kikanda na kimataifa. Mkakati huu unahusu mazao, mifugo, uvuvi na minyororo ya thamani inayohusiana nayo.

3. Kwa nini Mkakati wa Kilimo Ikolojia Hai ni muhimu? _____

Kilimo Ikolojia Hai kinaweza kusaidia:

- i. Kuongeza uzalishaji wa chakula;
- ii. Kuboresha afya na rutuba ya udongo;
- iii. Kuhifadhi mazingira na bioanuai;
- iv. Kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi;
- v. Kupunguza gharama za uzalishaji;
- vi. Kutoa chakula salama na chenye lishe;
- vii. Kuongeza kipato cha wakulima;
- viii. Kupanua ajira kwa vijana na wanawake;
- ix. Kuhifadhi mbegu na mifugo ya asili;
- x. Kufungua masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

4. Nini Maana ya Kilimo Ikolojia hai? _____

Kilimo Ikolojia hai kinaendana na asili. Kinachanganya mazao, mifugo na miti, kulinda afya ya udongo, maji na viumbe hai kwa njia endelevu. Mfumo huu unalenga kuzalisha chakula salama kwa kutumia rasilimali za asili kwa uangalifu na kupunguza utegemezi wa kemikali za viwandani.

Kilimo Ikolojia Hai kinahusisha:


- i. Matumizi ya mbolea asilia – Mbolea ya mboji, samadi, na mbolea ya kijani;
- ii. Kilimo mseto – Kupanda mahindi na maharagwe, mboga mboga na miti kwa pamoja;
- iii. Udhibiti wa asili wa wadudu waharibifu – Mwarobaini, majivu, mimea ya kuvutia wadudu (trap crops), na wadudu wenye manufaa badala ya kemikali;
- iv. Kuhifadhi mbegu za asili – Kutumia na kuboresha mbegu za kienyeji zinazoendana na mazingira yetu;
- v. Kufunika udongo – Kuweka matandazo ili kuzuia mmomonyoko na kuhifadhi unyevu
- vi. Ufugaji na kilimo – Kutumia mbolea kuboresha rutuba ya udongo kwa ajili ya mazao ambayo baadaye hutumika kulisha mifugo
- vii. Matumizi ya maji na ardhi kwa uangalifu na kwa njia endelevu

5. Dira ya Mkakati _____

Kuongoza uhifadhi wa mazingira, afya ya binadamu, ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, usalama wa chakula na lishe, maisha ya wakulima na ukuaji wa uchumi kupitia Kilimo Ikolojia Hai.

6. Dhamira ya mkakati _____

Kuandaa na kutekeleza miongozo ya kisera inayofaa kuinua uwekezaji na ubia katika kuendeleza Kilimo Ikolojia Hai kwa kujenga uwezo katika utafiti, kuongeza uelewa, mafunzo, huduma za ugani, usindikaji, usimamizi wa mnyororo wa uzalishaji na maendeleo ya soko katika Kilimo Ikolojia Hai ili kuongeza upatikanaji wa masoko ya ndani na kimataifa.



7. Lengo kuu la Mkakati

Kuchochea maendeleo ya sekta ndogo ya Kilimo Ikolojia Hai na kuingiza katika mfumo wa taifa wa maendeleo ya sekta ya kilimo ili kuimarisha uhifadhi endelevu wa mazingira kwa ajili ya kuboresha afya, mapato na usalama wa chakula ifikapo 2030.

8. Maeneo 12 ya kimbakati

8.1. Utafiti, mafunzo na huduma za ugani

Mkakati huu utaimarisha taasisi za utafiti, vyuo vikuu, vyuo na huduma za ugani ili wakulima wapate maarifa ya vitendo na ya kuaminika.

Hatua zilizopangwa ni pamoja na:

- i. Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima
- ii. Kuanzisha mashamba ya mfano
- iii. Kusaidia utafiti kuhusu wadudu, magonjwa, udongo, mbegu na masoko
- iv. Kuchanganya maarifa ya asili na utafiti wa kisayansi
- v. Kusambaza mbinu bora za kilimo kwa wakulima

8.2. Pembejeo na zana bora za kilimo ikolojia hai


Mkakati utahakikisha wakulima wanapata pembejeo bora, salama na zinazofaa, zikiwemo:

- i. Mbegu na vipando vya kilimo-hai
- ii. Aina za mifugo za kienyeji na vifaranga vya samaki
- iii. Mbolea ya mboji na mbolea-hai
- iv. Viuatilifu vya asili
- v. Zana na mashine ndogo za kilimo
- vi. Teknolojia za kuchakata pembejeo za kilimo-hai

Mkakati huu pia unaunga mkono uzalishaji wa ndani wa pembejeo za kilimo-hai na mashine.

8.3 Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kilimo

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) itatumika kusambaza taarifa kupitia: Simu za mkononi na mifumo ya kidijitali; redio na televisheni na mitandao ya kijamii. Usambazaji wa taarifa pia utafanyika kupitia mashamba darasa; siku za mkulima; machapisho; Mifumo ya taarifa za masoko; pamoja na mafunzo na kampeni za kuongeza uelewa kwa umma. Lengo ni kuwasaidia wakulima kufahamu nini cha kuzalisha, jinsi ya kuzalisha, na wapi wauze mazao hayo.



8. Maeneo 12 ya kimkakati

8.4. Kuimarisha ushirikiano na uratibu

Mkakati huu utaimarisha ushirikiano na uratibu miongoni mwa: Wizara na mashirika ya Serikali; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Wakulima na vyama vya ushirika; Taasisi za utafiti na mafunzo; Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mashirika ya kiraia; Makampuni binafsi; Taasisi za kifedha; Washirika wa maendeleo; na mashirika ya vyombo vya habari. Baraza la Kilimo Ikolojia Hai na Kitengo cha Uratibu vinapendekezwa kuundwa ili kusimamia utekelezaji.

8.5: Kuimarisha viwango na kupunguza gharama za uthibitishaji

Uthibitishaji huwasaidia watumiaji kutambua bidhaa za kilimo ikolojia hai na kuwawezesha wakulima kufikia masoko yenye thamani ya juu. Mkakati huo utasaidia:


- i. Kukuza viwango vya kilimo hai vya Afrika Mashariki
- ii. Kuimarisha Mifumo ya Dhamana Shirikishi
- iii. Kusaidia uthibitishaji wa makundi ya wakulima
- iv. Kuandaa alama au muhuri wa ubora wa kilimo ikolojia hai
- v. Kujenga uwezo wa kitaifa wa uthibitishaji
- vi. Kupunguza gharama za uthibitishaji
- vii. Kuboresha mifumo ya ukaguzi na uhakiki

8.6. Kuimarisha minyororo ya thamani na usindikaji

Bidhaa nyingi za kilimo hai huuzwa zikiwa ghafi. Mkakati huu utawawezesha wakulima kuvuka hatua ya uzalishaji wa malighafi pekee na kufikia masoko yanayofaa kwa kuimarisha usindikaji na ufungashaji; uhifadhi na usafirishaji; uwekaji nembo/lebo; udhibiti wa ubora; uendelezaji wa bidhaa; mifumo ya uzalishaji; vyama vya ushirika vya wakulima; pamoja na uhusiano kati ya wazalishaji, wasindikaji, na wanunuzi. Hii itawasaidia wakulima kupata faida kubwa zaidi kutokana na bidhaa kama vile kahawa, pamba, viungo, matunda, mboga mboga, kakao, na vyakula vya asili.

8.7 Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa hali ya hewa

Mkakati huu utahimiza mbinu za kiasili za kuhifadhi mazingira, zikiwemo: kilimo-misitu; uhifadhi wa udongo na maji; urejeshaji wa ardhi iliyoharibika; kulinda maeneo oevu na vyanzo vya maji; uhifadhi wa bayoanuwai; mbinu za kiasili kama vile Ngitili na kilimo cha Ngoro; na matumizi ya mbegu za asili.



8. Maeneo 12 ya kimbakati

8.8. Ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum

Mkakati utahakikisha wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalumu wanashiriki kikamilifu katika kilimo ikolojia hai. Usaidizi huo utajumuisha: mafunzo ya ujuzi na ujasiriamali; upatikanaji wa ardhi na fedha; fursa za kilimo cha kidijitali; usindikaji na uongezaji thamani; fursa za ajira na biashara ya kilimo; pamoja na ushiriki katika vikundi vya wakulima na vyama vya ushirika.

8.9. Kuwezesha upatikanaji wa fedha na uwekezaji


Wakulima wengi hushindwa kuwekeza kwa sababu ya ukosefu wa mitaji na mikopo nafuu. Mkakati utahimiza:

- i. Kuanzishwa kwa huduma za fedha zinazofaa wakulima;
- ii. Kuanzisha Vikundi vya akiba na mikopa;
- iii. Upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu;
- iv. Kutoa mafunzo ya kuongeza uelewa wa kifedha na biashara
- v. Kuanzisha Vyama vya Ushirika imara
- vi. Kuanzisha Mfuko wa Kilimo Ikolojia hai
- vii. Uwekezaji wa sekta binafsi.

8.10. Umwagiliaji na usimamizi wa maji

Mabadiliko ya tabianchi yameongeza ukame na mvua zisizotabirika. Mkakati huu utakuza upatikanaji wa maji ya uhakika ili kusaidia uzalishaji wa mwaka mzima na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Maeneo ya yatakayozingatiwa ni pamoja na:

- i. Kutambua vyanzo vya maji vinavyofaa
- ii. Teknolojia za umwagiliaji zenye gharama nafuu
- iii. Uvunaji na uhifadhi wa maji
- iv. Vikundi vya wakulima wanaotumia maji
- v. Mafunzo kuhusu usimamizi wa maji
- vi. Sheria ndogo za eneo husika kwa ajili ya matumizi endelevu ya maji
- vii. Mifumo ya umwagiliaji inayofaa kwa kilimo kinachozingatia ikolojia



8. Maeneo 12 ya kimbakati

8.11. Upatikanaji na matumizi ya ardhi

Ardhi ni msingi wa Kilimo Ikolojia Hai. Wakulima wanahitaji ardhi ya uhakika na inayofaa kwa ajili ya kilimo ikolojia hai. Mkakati utahimiza:

- i. Kutambua ardhi inayofaa;
- ii. Kutenga ardhi kwa matumizi maalum;
- iii. Kulinda mipango ya matumizi bora ya ardhi ;
- iv. Kuwapatia ardhi wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalumu;
- v. Kupunguza migogoro ya ardhi; na
- vi. Kulinda haki za umiliki wa ardhi.


8.12: Kuimarisha biashara na upatikanaji wa masoko

Mkakati huu unalenga kupanua masoko ya bidhaa za kilimo hai nchini Tanzania, Afrika Mashariki na kimataifa. Mipango iliyopangwa ni pamoja na:

- Kuanzisha na kuimarisha masoko ya ndani
- Kuwaunganisha wakulima na wanunuzi na wasindikaji
- iKuboresha taarifa za masoko
- Kutangaza bidhaa za kilimo hai katika maduka makubwa, hoteli na migahawa
- Kusaidia utangazaji wa mauzo ya nje
- Kuhimiza uwekezaji katika minyororo ya thamani ya kiikolojia
- Kutengeneza bidhaa zinazokidhi mahitaji ya soko
- Kupitia kodi na taratibu za biashara
- Kutangaza bidhaa za kilimo hai katika taasisi za umma kama vile shule, hospitali na vyuo vikuu


9. Malengo ya Utekelezaji wa Mkakati ifikapo 2030

Na.	Maelezo ya lengo	Idadi ifikapo mwaka 2030
1	Wakulima wamefikwa na maarifa ya kilimo ikolojia hai	3,000,000
2	Maafisa ugani wamepatiwa mafunzo	5,000
3	Mashamba ya mfano yameanzishwa	1,000
4	Taasisi au viwanda vinavyozalisha pembejeo za kilimo hai	50
5	Wakulima wanatumia kwa uhakika pembejeo za kilimo hai	1,000,000
6	Benki za mbegu za jamii zimeanzishwa	100
7	Mbegu za kienyeji na sampuli za rasilimali za kijenetiki zimehifadiwa	1,000
8	Wahusika katika mnyororo wa thamani wamepatiwa mafunzo au kuthibitishwa	1,000,000
9	Vyama vya ushirika vimeimarika	500
10	Masoko ya bidhaa za kilimo hai yameanzishwa au kuimarishwa	100
11	Maeneo ya ardhi ya kilimo ikolojia hai yameanzishwa	Maeneo 100
12	Wazalishajiwa bidhaa za kilimo ikolojia hai wameunganishwa na masoko	1,000,000
13	Vijana wamewezeshwa	2,000,000




9. Malengo ya Utekelezaji wa Mkakati ifikapo 2030

Na.	Maelezo ya lengo	Idadi ifikapo mwaka 2030
13	Vijana wamewezeshwa	2,000,000
14	Wanawake wamewezeshwa	3,000,000
15	Watu wenye mahitaji maalum wamesaidiwa	500,000
16	Mifumo ikolojia na mbinu himilivu asilia zimeongezeka	20
17	Wakulima wamesaidiwa kutumia umwagiliaji	Wakulima 1,000,000
18	Asilimia za gharama za uthibitishaji zimepungua	30%
19	Mfuko wa kilimo ikolojia hai umeanzishwa	1




10. Nani watekelezaji wa mkakati?

Na.	Wahusika wakuu	Majukumu
1	Serikali	• Kuweka sera, sheria na miongozo; • Kuratibu wadau; • Kutenga fedha; • Kutoa huduma za ugani; • Kuimarisha utafiti; • Kusimamia viwango na uthibitishaji; • Kuwezesha upatikanaji wa ardhi na masoko
2	Mamlaka za Serikali za Mitaa	• Kuingiza Kilimo Ikolojia Hai katika mipango ya maendeleo; • Kutoa ardhi; • Kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi; • Kutoa huduma za ugani; • Kusaidia masoko na miundombinu; • Kuelimisha jamii.
3	Wakulima na vyama vya ushirika	• Kutumia mbinu bora na salama; • Kuhifadhi udongo, maji na mazingira; • Kushiriki katika vikundi na vyama vya ushirika; • Kuhifadhi mbegu za asili; • Kuweka kumbukumbu za uzalishaji; • Kuzingatia viwango vya ubora; • Kushiriki katika mafunzo na tafiti.




10. Nani watekelezaji wa mkakati?...

Na.	Wahusika wakuu	Majukumu
4	Taasisi za utafiti na mafunzo	• Kufanya utafiti • Kubuni na kuendeleza teknolojia zinazofaa • Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima • Kuweka kumbukumbu za maarifa asilia • Kufanya majaribio ya pembejeo za kiikolojia na mbinu za kilimo
5	Sekta binafsi	• Pembejeo za kiikolojia • Utengenezaji na usambazaji wa zana ya kilimo • Uchakataji na ufungashaji • Uthibitishaji • Uhifadhi na usafirishaji • Huduma za kidijitali; • Kutoa huduma za kifedha na uendelezaji wa masoko
6	Mashirika yasiyo ya kiserikali	• Uhamasishaji wa jamii • Mafunzo na uelimishaji • Utafiti na uvumbuzi • Uunganishaji na masoko • Kujenga uwezo • Kutafutaji wa rasilimali fedha • Kusambaza matokeo ya miradi yenye mafanikio



10. Nani watekelezaji wa mkakati?...

Na.	Wahusika wakuu	Majukumu
7	Vyombo vya habari	• Kusambaza taarifa za kilimo ikolojia hai • Kutangaza bidhaa zinazozingatia kilimo ikolojia hai • Kutangaza fursa za kibiashara • Kurekodi taarifa za mafanikio • Kuunganisha wakulima, walaji na masoko
8	Walaji	• Kununua bidhaa salama na zilizothibitishwa; • Kuthamini bidhaa za wakulima; • Kuhamasisha matumizi ya chakula chenye lishe; • Kutoa mrejesho kuhusu ubora na upatikanaji wa bidhaa.



11. Bajeti

Makadirio ya bajeti ya kutekeleza mkakati huu ni TZS 52,729,340,575. Ufadhili unatarajiwa kutoka katika mgao wa bajeti ya Serikali; washirika wa maendeleo na wafadhili; uwekezaji wa sekta binafsi; taasisi za kifedha; mashirika ya wakulima na vyama vya ushirika; mifuko ya hali ya hewa na bayoanuwai; mapato yatokanayo na masoko na huduma za uthibitishaji; Hafla za uchangiaji wa fedha; na kupitia mashirikiano.

12. Ufuatiliaji na tathmini

Utekelezaji wa Mkakati utafuatiliwa kupitia:

- Ripoti za robo mwaka;
- Ripoti za mwaka;
- Tathmini ya muda wa kati;
- Tathmini ya mwisho;
- Mikutano ya wadau;
- Ukusanyaji wa takwimu;
- Ziara za ufuatiliaji; na
- Utafiti na tathmini za mafanikio.

13. Ujumbe kwa wananchi

Kilimo Ikolojia Hai ni jukumu la kila mmoja. Wakulima, Serikali, wafanyabiashara, watafiti, walaji na taasisi zote wanapaswa kufanya kazi pamoja.

Kwa kutumia Kilimo Ikolojia Hai:

- Tutapata chakula salama leo na kesho;
- Tutahifadhi ardhi na maji;
- Tatalinda mazingira;
- Tutapunguza gharama za kilimo;
- Tutaongeza kipato cha familia;
- Tutafungua ajira na masoko;
- Tutafanya kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi.

“Kilimo Ikolojia Hai kitahakikisha tunapata chakula leo na kesho huku tukihifadhi mazingira”



HITIMISHO

Kipeperushi hiki ni toleo lililorahisishwa na kuwekwa katika mfumo wa vitendo wa Mkakati wa Kitaifa wa Kilimo Hai na Ikolojia ya Kilimo (NEOAS), lililoandaliwa ili kuwezesha upatikanaji na matumizi mapana zaidi ya maarifa yanayohusiana na NEOAS.

Kwa msaada wa:

Mradi wa Kitovu cha Maarifa ya kilimohai cha Afrika Mashariki kuhusu Kilimo ikolojia hai o Afrika Mashariki (KHEA)

Kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Tanzania

Kimezingatia:

Mkakati wa Kitaifa wa Kilimo Hai na Ikolojia ya Kilimo (NEOAS)

Pata maarifa zaidi:

Jukwaa la Kidijitali la KCOA

<https://kcoa-africa.org/>

